www.repoa.or.tz

Toleo Na 2/2019 Mei, 2019

# Dokezo la Utafiti

POLICY RESEARCH REPOA FOR DEVELOPMENT

# Sera za Kilimo na Jitihada za Kupunguza Umaskni Tanzania

*Na: Paschal B. Mihyo*

## Utangulizi

Kitabu hiki kina sura saba ambazo zinaangalia sera mabali mbali kuhusu maendeleo vijijini na mchango wake kwenye kupunguza umaskini Tanzania. Kinaanza na sera zilizotungwa na kuetekelezwa kipindi cha Ujamaa na Kujijetegemea. Kina sura nyingine zinazo angalia mchango wa elimu kwenye ufanisi wa kilimo; mradi wa matrekta madogo aina ya 'power tillers' kwenye baadhi ya wilaya; awamu tatu za sera za ruzuku za pembejeo kwa wakulima wadogo; na kilimo cha tumbaku na hatima yake kutokana na mabadiliko kwenye soko na sera za kimataifa kuhusu zao hilo. Pia kuna sura moja inayolinganisha mbinu za ukuzaji mnyororo wa thamani kwenye zao la korosho nchini Tanzania na Vietnam na nyingine ambayo inagusia mambo muhimu ya kufanikisha ushirikiano kati ya taasisi za kiserikali na asisi zisizo za kiserikali katika kutekeleza na kufanikisha sera za kilimo nchini Tanzania.

### Ujamaa na Uzalishaji wa Pamoja Tanzania vijijini (Imeandikwa na Paschal Mihyo)

Sera nyingi zilizobuniwa na kutekelezwa katika kipindi cha uongozi wa Baba wa Taifa wa Tanzania Mwalimu Julius Nyerere, zilitilia mkazo sana mendeleo vijijini kupitia sera ya Ujamaa na Kujitegemea ambayo nia yake ilikuwa ni kuondoa mifumo ambayo ilikuwa inaendeleza umaskini na dhuluma kwa walio wengi. Alivunja mfumo wa kikabaila na kupitisha Azimio la Arusha la 1967 ambalo lilikuwa sera msingi ya maendeleo ya kijamaa yanayosimamiwa na dola. Utekelezaji wake ulianza na makazi ya vijiji vya hiari vilivyokuwa vinasimamiwa na wanavijiji. Kasi ya makazi haya ilivyoanza kupungua watu walihamishiwa kwenye vijiji vilivyotayarishwa na serikali. Lakini sera hii mpya haikufanikiwa kwa sababu mbali mbali. Kwanza, watu wengi walihamishwa kutoka makazi yao ya jadi na hili halikuwapa sana motisha. Pili, kwa vile wengi walihamishwa kwa nguvu, walianza kuuchukia mpango mzima. Tatu, ingawaje Rais Nyerere alikuwa na imani na dhana ya ushirikishwaji wa raia, utekelezaji wa mpango wa kuhamia vijijini ulitumia nguvu kwa sababu watekelezaji hawakuwa na imani na dhana ya ushirikishwaji wa raia kwenye maamuzi yanayogusa maisha yao. Nne, sera hiyo na utekelezaji wake vilijikita kwenye dhana ya kwamba jamii za Kiafrika zilijengwa kwenye misingi ya ujima na ushirika katika kuzalisha na kugawa matokeo ya uzalishaji wakati misingi hiyo iliishaanza kumomonyoka na misingi ya ubinafsi na ubepari kujikita hata kabla ya uvamizi wa kikoloni. Kwa sababu hizi nne, sera za Ujamaa hazikufanikiwa kuondoa umaskini au kuongeza mafanikio kama ilivyotarajiwa nchini kote.

### Elimu na Kilimo chenye Tija Tanzania Vijijini (Imeandikwa na Lucas Katera[1])

Sura hii ya kitabu inatoa matokeo ya uchambuzi wa kitaalam kuhusu mchango wa ujuzi utokanao na mfumo rasmi wa elimu na ule usio rasmi, kupatikana kwa ardhi na mikopo, kwa ujuzi na ufanisi wa kilimo. Uchanganuzi uliofanywa unadhihirisha umuhimu wa elimu ya msingi, elimu ya jadi, upatikanaji wa ardhi na mikopo nauzoefu wa muda mrefu kwenye kuogeza tija kwenye kilimo. Takwimu kuhusu mchango wa elimu kwenye ubunifu na urahisi wa kuitumia teknolojia zinaonyesha kwamba mkulima akiwa na kiwango cha elimu rasmi kufikia miaka sita, kukiambatana na kuwa na nyenzo za kuzalishia na uzoefu kwenye masuala ya hifadhi ya ardhi na uzoefu wa muda mrefu wa kilimo, anajengewa mazingira ya kuongeza ufanisi kwenye kilimo na kuondokana na umaskini. Takwimu zinaonesha pia kwamba ni wakulima wadogo wachache wanaowekeza kwenye vichochea tija kwenye kilimo kama udhibiti wa mmomonyoko wa ardhi na uvunaji wa maji (10%), upandaji wa miti (13%) au matumizi ya ushauri wa maofisa ugani (36%). Takwimu zimeonesha pia kwamba wakulima waliowekeza kwenye kudhibiti mmomonyoko wa udongo na uvunaji wa maji, walivuna wastani wa kilo 886 ukiwalinganisha na wale ambao hawakuwekeza kwenye nyenzo hizo waliovuna kilo 618 tu kwa eka. Wenye mavuno ya wastani wa kilo 880 walikuwa pia wamepanda miti kwenye mashamba yao ukilinganisha na kundi la pili ambao hawakupanda miti. Wakulima waliotumia utaalam wa maofisa ugani walivuna kwa wastani kilo 747 tofauti na wale ambao hawakuutumia utaalam huo waliovuna kwa wastani kilo 586 tu.

1 Dr. Lucas Katera ni Mtafiti mwandimizi na Mkurugenzi wa Utafiti wa Kimkataba REPOA.

**Jedwali Na.1: Wastani wa Mavuno Kwa Kila Mbinu ya Uzalishaji (kilo za mahindi)**

| | Ndiyo | Hapana |
|---|---|---|
| Waliodhibiti mmomonyoka na kuvuna maji | 886.4 | 617.8 |
| Waliopanda miti kwenye mashamba | 880.3 | 608.4 |
| Walitumia utaalam wa Ofisa Ugani | 747.0 | 586.0 |

Matokeo ya utafiti yanaonesha pia kwamba elimu rasmi na ile ya jadi au itokanayo na mfumo usio rasmi zote huchangia uwezo wa mkulima kubuni na kuiga mbinu mpya za uzalishaji na wakulima wakipewa mafunzo kwa muda wa kutosha hupata uwezo wa kubuni na kuiga mbimu mpya za uzalishaji. Aidha utafiti umeonesha kwamba ingawaje upatikanaji wa mikopo peke yake hausaidiii kuongoza au kubadili maamuzi ya wakulima kuhusu kupunguza mmomonyoko au kuvuna maji na kupanda miti, unasaidia kwenye kuongeza matumizi ya utaalam utokanao na maofisa ugani.

Funzo kubwa litokanalo na utafiti huu ni kwamba elimu rasmi ya shuleni na ile ya jadi zote ni muhimu kwa kujenga uwezo wa wakulima kubuni na kujifunza mbinu mpya za kilimo kwa sababu elimu ya shuleni inamjengea mkulima stadi za kusoma na kuhesabu ambazo zinamsaidia kumudu na kuona umuhimu wa ubunifu na mageuzi kwenye kilimo, wakati elimu ya jadi inamsaidia kuzitumia mbinu hizo kwenye mazingira halisi aliyo na uzoefu nayo. Funzo la pili ni kwamba shabaha ya kujitosheleza kwa chakula nchini itaendelea kutuhadaa ikiwa changamoto za kuwafikishia huduma za elimu wakulima hazitatafutiwa ufumbuzi wa kutosha.

## Ubunifu wa Gharama Nafuu Unaolenga Maendeleo Shirikishi: Tafiti Kifani Kuhusu Ukulima Kutumia trekta ndogo 'Power Tillers' Nchini Tanzania. (Imeandikwa na Donald Mmari[2] na Sylvester Mpanduji[3])

Utafiti huu ulifanywa kutathmini na kuchunguza mazingira yanayofaa kwa ubunifu wenye gharama ndogo wa kutumia trekta ndogo zijulikanazo kama 'power tillers' kuchochea mabadiliko ya kilimo barani Afrika hasa nchini Tanzania. Utafuti huu kifani unatoa uchanganuzi wa mifumo na michakato ya kitaasisi inayosaidia au kutosaidia upokeaji na matumizi ya ubunifu unaoambatana na matumizi ya trekta hizi ndogo hasa kwa kuzingatia mchango wake kwenye kuboresha kilimo. Zilichaguliwa wilaya mbili zenye 'trekta hizi ndogo kwa wingi kwenye mikoa miwili ya Morogoro na Mbeya, yaani wilaya ya Kilombero and wilaya ya Mbarali.

Mchakato wa kuingiza, kujenga uzoefu na uwezo wa kutunza na kukarabati trekta hizi mpya ulikuwa na changamoto mbali mbali. Kwanza ilikuwa kwamba wakati wa kuchagua trekta za kuagiza watumiaji wengi walivutiwa na unafuu wa bei na siyo ubora wa trekta na nyingi zilizoagizwa zilikosa vipuli vinavyofaa. Pili trekta hizo hazikuundwa ili zitumike kwenye mazingira ya mikoa husika. Matokeo yake ni kwamba nyingi zilifanyiwa mabadiliko ya kiufundi ambayo pia hayakuziongezea ubora. Tatu ni kwamba trekta hizo zilitumiwa kufuatana na mazoea na matakwa ya wakulima zikiwemo shughuli zisizolingana na uwezo wake. Matumizi haya yalisababisha trekta nyingi kutodumu kwa muda mrefu. Hata hivyo, wakulima wengi walizitumia kupunguza matatizo yao kwenye kilimo na shughuli zingine tofauti na kilimo kama ilivyoonyeshwa kwenye Jaedwali Na.2 hapo chini.

**Jedwali Na. 2: Matumizi ya 'power tillers' wilaya za Mbarali na Kilombero**

| | Matumizi | Mbarali | | Kilombero | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wahojiwa | % | Wahojiwa | % |
| 1 | Kulimia | 60 | 100 | 7 | 17 |
| 2 | Kusafirishia | 46 | 77 | 31 | 66 |
| 3 | Kumwagilia | 6 | 10 | 0 | 0 |
| 4 | Kukoboa | 2 | 3 | 0 | 0 |
| 5 | Kusagia | 0 | 0 | 8 | 17 |

**Kutokana na**: Takwimu za utafiti


Utafiti unaonesha pia kwamba ingawa matokeo yanatofautiana wilaya hadi wiliya, katika wilaya zote matumizi ya hizi trekta ndogo yalipunguza gharama za usafirishaji, uzalishaji uliongezeka na maeneo yaliyolimwa yaliongezeka kwa zadi ya asili mia 80 ya wakulima waliohojiwa. Funzo kubwa litokanalo na utafiti huu ni kwamba miradi inayolenga wakulima ni vigumu kufanikiwa kama inavotegemewa ikiwa maamuzi yanafanywa bila kuwahusisha kwa sababu maamuzi ya kutoka juu yanawanyima wakulima nafasi ya kuchagua, kuzoea, kumudu na kuzitunza teknoljia mpya ingawaje mashine kama hizi trekta ndogo zinawavutia sana vijana na zina uwezo mkubwa wa kusaidia ongezeko la ajira na kupunguza matumizi ya nyenzo duni miongoni mwa wakulima.

Inapendekezwa kwamba katika kupanga mikakati ya mageuzi ya kilimo kuna umuhimu wa kutumia mbinu za sayansi ya siasa ya kiuchumi ili kuwianisha mahitaji mbali mbali ya wakulima na mikakati ya kuwainua kiuchumi. Inapendekezwa pia kufanyike utafiti zaidi kuhusu taratibu za kutengeneza mikakati kuhusu ubunifu wa mbinu za uzalishaji zinazopunguza gharama kwa wakulima na zinazoweza kutumika kwa urahisi katika mazingira ya wilaya mbali mbali Tanzania ambazo ni rafiki kwa watumiaji na zenye gharama nafuu kwa wale walioko chini sana kwenye kilimo vijijini.


## Mchango wa ruzuku ya kilimo kwa wakulima wadogo wenye kipato cha chini: Changamoto na mafunzo yatokanayo na Mpango wa Taifa wa Ruzuku za Pembeneo nchini Tanzania (Imeandikwa na Cornel Jahari[5])

Sera zinazohusu ruzuku kwa wakulima wadogo zimekuwepo nchini Tanzania tangu muongo wa kwanza wa uhuru na zimehusisha mikakati mbali mbali. Suala kubwa lilioongoza utafiti huu ni: kwa jinsi gani taratibu na mipango ya usimamiaji, usambazaji, na utumiaji wa ruzuku kwenye kilimo zinasaidia au kuathiri uzalishaji na tija kwenye kilimo cha wakulima wadogo? Matokeo ya utafiti kuhsu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Ruzuku za Pembejeo uliozinduliwa mwaka 2008 ukiwa umelenga wakulima wadogo wenye kipato cha chini sana, yanaonesha kwamba sera hiyo ruzuku haikuleta mabadiliko makubwa kwenye kilimo na matokeo yake kwa ujumla. Kiwango cha mabadiliko kwenye sekta ya kilimo kwa ujumla yamekuwa madogo sana yakiwa kwenye kiwango cha asilimia 4 kwa wastani kwa kipindi kirefu (2002 hadi 2011) kama inavyooneshwa kwenye kielelezo Na.1 hapo chini.

**Kilelezo Na. 1: Kiwango cha Ongezeko la Uzalishaji Kwenye Kilimo kwa Mwaka (Kwa bei za 2001)**




2 Dr. Donald Mmari ni Mtafiti Mwandamizi na Mkurugenzi Mtendaji, REPOA
3 Engineer Sylvester Mpanduji is Mhadhiri Mwandamizi Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (SIDO) Tanzania.




**Source:** Adopted from National Account (URT 2012)

***Tija kutokana na ardhi***

Ingawaje kumekuwa na ogezeko kubwa kwenye uzalishaji wa mazao ya chakula nchini Tanzania, hakukuwa na tofauti kubwa kitakwimu kati ya kipindi kabla na baada ya kuzinduliwa kwa mpango huu. Inaonekana pia kwamba mazao ya mpunga na mahindi hayakuweza kukidhi mahitaji ya usalama wa chakula na lishe kama ilivyotarajiwa ukiyalinganisha na mazao mengine kama viazi vitamu. Lakini matokeo yote kwa ujumla yanaonesha kwamba ruzuku imewasaidia kwa kiasi kikubwa wakulima wadogo waliotapata vocha za ruzuku na kuzitumia kununua mbegu za kisasa na mbolea kwani waliweza kuvuna magunia saba ya kilo mia moja ya mahindi kwa wastani kwa ekari moja wakati wale ambao hawakutumia mbegu za kisasa wala mbolea walivuna magunia 4.4 ya mahindi kwa wastani kila ekari moja. Mbali na mafanikio hayo, mpango huo unaonekana haukuwanufaisha walengwa wote kwa sababu ingawa wengi wao walijua kwamba mpango huu upo, uelewa wao kuhusu stahiki zao, nafasi za kushiriki, vigezo vya kuwasaidia washiriki na muda wa kuanza na kuisha mpango huo ulikuwa mdogo. Pia mchakato wa kutambua, kuchambua na kuchagua wanaostahili kunufaika haukuwa na uwazi wa kutosha.

Inapendekezwa kufanyike tathmini ya vigezo vinavyotumika kuchagua walengwa ili kuhakikisha wakulima wadogo wenye kipato cha chini sana wananufaika. Pia inapendekezwa vyama vya ushirika vifanyiwe mabadiliko ili kuviongezea uwazi kwenye taratibu zake zinazohusu usambazaji wa pembejeo na pia kuwasaidia wakulima kuuuza mazao yao kwenye masoko mbali mbali bila matatizo.

## Uchambuzi wa Ushindani Kwenye Mnyororo wa Thamani wa Tumbaku Ndani na Nje ya Nchi (Imeandikwa na Jamal B. Msami4, Moses Tekere[5] na Calvin Manduna[6])

Sekta ya tumbaku inawahusisha takriban watu milioni 1.45 na huchangia kwa wastani asilimia 29 kwa pato litokanalo na mauzo ya bidhaa nje ya Tanzania. Lakini licha ya mchango huu sekta hii imechangia kwa kasi kikubwa uharibifu wa mazingira kutokana na ukataji wa miti na mazao ya tumbaku yana athari kubwa kwa makundi mengi ya watu wakiwemo wapandaji, wavutaji na wasiovuta tumbaku. Nchini Tanzania kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu hatima ya tumbaku. Kuna watumiaji wa tumbaku takriban milioni 2.88 (wakiwemo watoto wapatao 50,000), na watu wapatao 6,800 hufariki dunia kila mwaka kutokana na matumizi ya tumbaku. Tafiti mbali mbali zinaonyesha kwamba asilimia 32 ya vifo vitokanavyo na saratani nchini husababishwa na matumizi ya tumbaku. Wanaharakati wanaopinga uvutaji wa tumbaku wametoa mwito kwa serikali kuongeza ukali kwenye sheria ya mazao ya tumbaku ya mwaka 2003 (Tobacco Products (Regulation) Act, 2003).

Kuhusu dhamana ya kilimo swala kubwa linahusu ufyekaji holela wa misitu na mmomonyoko wa ardhi utokanao na ukulima wa tumbaku na matumizi ya kuni kwenye kuboresha tumbaku. Ufyekaji wa misitu unapunguza rutuba ya ardhi inayohitajika kwa mazao ya chakula; hupunguza hazina ya misitu kwa ajili ya mbao na matumizi mengine kama kupikia na ujenzi. Madhara mengine yatokanayo na kilimo cha zao hili ni matumizi ya dawa za sumu za kuua wadudu ambazo huchafua maji yaliyoko chini ya ardhi.

Sekta ndogo ya tumbaku inakabiliwa na changamoto kadhaa kwenye maeneo ya mazingira na afya ya bindamu, matatizo ya ufanisi kwenye sera za mauzo na kiwango cha uzalishaji kwa ujumla. Mauzo ya kando yamepungua lakini bado yapo na kuna tatizo kwenye hali ya uongozi hasa poromoko la maadili katika vyama vya ushirika vya msingi. Mapungufu yoyote kwenye uendeshaji wa vyama vya ushirika yanaathiri utoaji wa mikopo, huduma za ugani na usambazaji wa nyenzo kwa wakulima. Gharama za uzalishaji nchini Tanzania ziko juu sana na zikichanganyika na kuteremka wa mauzo zinapunguza faida kwa wanunuzi ambao kwa sababu hiyo wanahamia kwenye masoko nafuu Malawi na Zambia. Uwekezaji pia ni tatizo. Mwaka 2015/16 ni asilimia 16 tu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya sekta hii zilitolewa na serikali na matokeo yake ni kwamba miradi kuhusu upimaji wa mashamba, utoaji wa hati miliki, utoaji wa ruzuku, ujenzi wa maghala na uwekezaji kwenye utafiti na huduma za ugani ulikuwa mdogo.

Hitimisho la utafiti huu ni kwamba sekta ndogo ya tumbaku iko kwenye njia panda na inakabiliwa na mabadiliko ambayo yatabadilisha matumizi ya zao lake siku chache zijazo na fikra na tabia za watu kuhusu tumbaku na ilihali tumbaku bado ina mchango mkubwa kwa kipato cha nchi kwa fedha za kigeni na mamilioni ya watu wanaitegemea, harakati za kukomesha uvutaji wa sigara pamoja na mikataba ya kimataifa kuhusu tumbaku zinaongeza utata kwenye hatima ya zao hili.

Kwa hiyo inapendekezwa kwa serikali kuchukua hatua amabazo zinaweza kuongeza ubora wa tumbaku na uwezo wa ushindani kwa zao hili kwenye masoko ya ndani na nje. Inapendekezwa pia kuwekeza kiasi cha kutosha kwenye miundombinu ya uchakataji wa tumbaku ili kuongeza thamani ya zao hili na pia kuanza kutafuta masoko mapya hasa Mashariki ya Kati na Asia ambako soko linaendelea kupanuka. Pia inapendekezwa kwa serikali kutengeneza mkakati wa muda mrefu utakaowasaidia wakulima kupanua wigo na mnyororo wa thamani wa mazao mbadala na kujikwamua kutoka kwenye utegemezi wa zao la tumbaku peke yake.

## Hadithi Kinzani za Minyororo ya Thamani: Tanzania na Vietnam (Imeandikwa na Blandina Kilama[7])

Sura hii ya kitabu inalinganisha minyororo ya thamani ya korosho nchini Tanzania na Vietnam na kutoa mafunzo kadhaa kwa Tanzania yatokanayo na jinsi Vietnam inavyosimamia maboresho ya zao la korosho katika mnyororo wa thamani nchini humo. Vietnam huangalia sera zake kwa kina na hutilia maanani maboresho kwenye uzalishaji, tija na maslahi ya wazalishaji tofauti na Tanzania ambako hatua nyingi hazitabiriki, tatizo ambalo limechangia kudorora kwa uzalishaji na maslahi ya wazalishaji. Uendeshaji wa masoko nchini Tanzania umechangia kwa kiasi fulani kuteremka kwa ubora na bei za mazao na kuwaweka wakulima kwenye kitu kinachoitwa kitaalaam, 'Mtanziko wa Wafungwa' ambao huleta msawazo hafifu wa ubora na tija ya mazao. Nchini Vietnam, usanifu wa ubunifu umewawezesha wakulima kuzalisha mazao bora na kupata bei nzuri kutoka kwa wachakataji. Utafiti huu wa korosho unaonesha kwamba uhuru wa wakulima Vietnam wa kuchagua unawapa wachakataji mbali mbali changamoto na unawafanya wachakataji washindane ilihali uhodhi wa chombo kimoja cha serikali kama ilivyo Tanzania, ni kikwazo kikubwa kwa ukuzi wa sekta nzima. Vietnam inaonesha kwamba masoko ambayo yanasaidiwa na serikali yanafanikiwa zaidi kuliko yanayosimamiwa moja kwa moja na serikali.

Ukiangalia mfano wa Tanzania ni rahisi kuona kwamba serikali ikisimamia moja kwa moja inaweza kukwaza kukua kwa sekta ya korosho. Serikali ya Vietnam pia inajihusisha kwenye sekta lakini kwa

4 Dr. Jamal Msami ni Mtafiti Mwandamizi na Mkurugenzi wa Tafiti za Kimkakati REPOA, Tanzania. Email: jamal@repoa.or.tz

5 TRADES Centre, Zimbabwe. Email: mtekere@tradescentre.co.zw

6 ACP International Trade Advisor, Washington DC. Email: cmanduna@gmail.com

7 Dr. Blandina Kilama ni Mtafiti Mwandamizi REPOA na Kaimu Murugenzi Mtendaji wa Economic Society of Tanzania

kutoa mbegu za kisasa, kutengeneza miundombinu, kueneza huduma za umeme, kusaidia utafiti na kusimamia viwango vya uchakataji. Dola yenye taasisi na mikakati madhubuti hutengeneza mazingira mazuri kusaidia sekta binafsi kushamiri na kuimarisha ubunifu kwa njia endelevu. Nchini Tanzania dola hutenga raslimali za uzalishaji zinazolenga kupunguza gharama za uzalishaji kwa wakulima tu na kwa muda mfupi na faida za mkakati huu huwa ni ndogo. Utaratibu wa mauzo ya korosho na pembejeo huhodhiwa na vyombo vya serikali ingawaje biashara ya kokwa za korosho imeachwa kwenye soko huria. Nchini Vietnam, korosho, pembejeo na kokwa vyote viko kwenye soko huria.

Suala la msingi kwenye hili siyo dola kuingilia tu, bali ni majukumu ya dola kwenye kufanya hivyo. Dola ikiwa kichocheo cha maendeleo inajitahidi kuwahusisha wadau wengine kutumia mahusiano ya nyuma na mbele kwenye msiamiati wa kiuchumi na kuhimiza ushirikiano wa wima na masula ya uchumi mkubwa yaani 'economies of scale'. Lakini uwekezaji wa dola ukilemea upande mmoja tu miongoni mwa wadau yaani uhusiano wa mbele au 'forward linkages' mafao kwa wadau hao hao yanapungua na matokeo yake ni masula ya uchumi hafifu yaani 'diseconomies of scale' kwa sekta yote. Changamoto zinazojitokeza kwenye sekta ya korosho ni pamoja na upungufu wa raslimali fedha na raslimali watu. Pia udhaifu unatokana na kushindwa kujenga sekta binafsi yenye uwezo mkubwa na kuendeleza mfumo ambao unaona ugumu kujibadilisha hasa kuhusu usambazaji wa pembejeo na zana nyingine.

Nchini Tanzania, mikataba ya papo hapo hufanyika kupitia taasisi za serikali na hii hupunguza ubora wa mazao na bei kwa wakulima. Kwa hiyo mtindo wa mauzo huwa na athari kwa wakulima na kuwaweka katika kile kinachoitwa 'Mtanziko wa Wafungwa', ambao kama ilivyosemwa awali huleta msawazo hafifu wa ubora na tija ya mazao. Mtanziko huu huwaathiri siyo tu wakulima bali pia wachakataji ambao wanaweza kutishiwa na upungufu wa korosho wakulima wakiacha kulima zao hilo na kulima mazao mbadala kama mpira na mengineyo.

Tatizo la mikataba ya papo hapo linaweza kutatuliwa na ongezeko la kuaminiana litokanalo na umaarufu wa wanunuzi na wauzaji. Nchini Vietnam kuaminiana kati ya pande hizo mbili hujengwa kwenye ngazi mbali mbali. Kukiweko na masula ya uchumi mkubwa au 'economies of scale' wakulima walio huru huwa wanatarajia kulipwa bei nzuri ili wasiache kulima mazao yao. Pia wachakataji wakubwa huwa wanazingatia sana viwango na huwa mfano kwa wachakataji wengine. Katika hali hii serikali huwa inawadhibiti wachakataji wakubwa wachache halafu wao wanawapa mikataba wachakataji wadogo. Katika hali hii pande zote kuaminiana ni muhimu sana.

Mwandishi anapendekeza upanuzi wa soko huria kwenye sekta ya korosho; mkakati wa kukuza sekta binafsi; ugatuzi wa shughuli za usambazaji wa nyenzo za uzalishaji na utanuzi wa aina ya mazao ili kupunguza utegemezi wa zao moja la korosho kwa wakulima na kuwaongezea sauti kwenye maamuzi yanayohusu mazao yao.

## Ushirikiano Bora Kati ya Serikali na Asisi Zisizo za Kiserikali Katika Kuondoa Umaskini Tanzania: Mifano Miwili (imeandikwa na Paschal B. Mihyo)

Sura hii inafanya upembuzi wa mahusiano kati ya asasi za kiserikali na zile zisizo za kiserikali hususan Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVAWITA) na Misali Conservation Association (MICA) iliyoko Pemba, Zanzibar. Asasi mbili hizi zimeweza kujenga misingi thabiti ya ushirikiano kati yake na serikali ambayo imezisaidia kutengeneza ulingo wa kuwasaidia wanachama wake kushirikiana na kuzishawishi serikali za wilaya kuwasaidia wakulima kupata ardhi na kuchangia mawazo ambayo yamezingatiwa na serikali katika mageuzi ya sera na kwa ujumla katika kupunguza umaskini. Mafanikio haya yametokana na asasi hizi kuwa na mizizi kwenye jamii, demokrasia katika uongozi wake, na mahusiano thabiti kati yake na serikali za mikoa, wilaya na mitaa ambavyo vimeziwezesha kupata sauti ya kutosha kwenye maamuzi ya vyombo vya ngazi za juu yanaogusa maisha, maslahi na shughuli za wanachama wao.

Pamoja na hayo MICA na MVIWATA zimekuwa na sifa zinazofanana ambazo zimeivutia serikali na vyombo vyake kushirikiana nazo. Zote mbili zinashughulika na uzalishaji kwenye maeneo yake na zina nia ya kuinua kiwango cha maisha cha wanachama wake. Zote mbili zinategemea zaidi raslimali za ndani ya nchi ingawaje zinafadhiliwa pia na mashirika ya nje. Zina kamati za misingi kwenye ngazi ya vijiji, kata na wilaya. Zimesaidia kuwashirikisha wanachama wake kwenye maamuzi muhimu na kuwapa sauti kwenye maamuzi yanayogusa maslahi yao. Pia asasi hizi hazijiingizi kwenye mambo ambayo hayapo kwenye mamlaka zake kwa mfano siasa na kadhalika. Sifa hizi chache zimezisaidia asasi hizi kujenga uhusiano na ushirikiano mzuri na serikali na kutimiza malengo yake na kuchangia sera. Mafanikio na taratibu zao ni funzo kubwa kwa asasi nyingine zisizo za kiserikali ambazo zingependa kuongeza mchango wake kwenye sera za nchi. Sura hii inahitimisha kwa kupendekeza kwamba serikali iongeze ushirikiano na asasi za kiraia; iongeze ufadhili kwa asasi za kiraia ili kuziondoa kwenye utegemezi kwa wafadhili wa nje na iweke vyombo maalum vitakavyosaidia kukutanisha vyombo vyake na asasi hizi za kiraia. Asasi hizi pia zinashauriwa kujiepusha na siasa kwa sababu shughuli hizo ni za vyama vya siasa.

REPOA
157 Mgombani/REPOA Street, Regent Estate
P.O. Box 33223, Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +255 22 2700083, Cell: +255 75 409 1677 Fax +255 22 2705738
Website: www.repoa.or.tz Email: repoa@repoa.or.tz

**Kituo cha Taarifa na Maarifa, REPOA**
Kituo chetu cha Taarifa na Maarifa kinatoa mazingira mazuri kwa utafiti wa fasihi na vitabu / maandiko mbali mbali kwa haraka na kwa urahisi wa matumizi ya maarifa na taarifa. Imeunganishwa na wavuti (internet) kwa ajili ya matumizi ya maktaba ya mkondoni (online) kuwasaidia wanaosomea Shahada za Uzamili na Uzamivu, watafiti na wasomi kwa kuwapatia magazeti, vitabu, ripoti n.k. ya siku za karibuni.

**Saa za Ufunguzi**
Kituo cha Taarifa na Maarifa kinakuwa wazi kuanzia Jumanne hadi Ijumaa saa 4.00 asubuhi hadi saa 7.00 mchana, saa 8.00 mchana hadi saa 11.00 alasiri. Maktaba ya mkondoni (online) ni wazi saa 24 kila siku.

@REPOA 2019
Matokeo, tafsiri, hitimisho, na maoni yaliyotolewa humu ndani ni ya mwandishi na siyo lazima yawe yanaakisi maoni na sera za REPOA.